



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. NA.50/77/04/69.

06.05.2024.

**WANANCHI WOTE**

**WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE.**

**YAH: TANGAZO LA UTUNGAJI WA SHERIA NDOGO.**

Mada tajwa hapo juu yahusika.

2. Kwa mujibu wa **kifungu cha 153 na 155 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287**, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia wananchi, wakazi, pamoja na wadau wote wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale kuwa; Halmashauri inakusudia kutunga **Sheria Ndogo ya (Uthibiti Utoro na Upatikanaji wa Chakula Elimu ya Msingi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, 2023**.
3. Kwa Tangazo hili, wananchi, wakazi pamoja na wadau wote wa Halmashauri hii mnaalikwa kujitokeza kutoa maoni, mapendekezo au pingamizi kuhusu rasimu ya Sheria Ndogo tajwa hapo juu.
4. Aidha, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji itafanya kikao cha kupokea maoni, mapendekezo na, au pingamizi hizo **tarehe 24/05/2024** kuanzia **saa 3:00 Asubuhi**, katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.
5. Pia, maoni, mapendekezo, na pingamizi zinaweza kuwasilishwa kwa maandishi katika Ofisi ya Mtendaji wa kata au Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) kwa mkono au kupitia anuani ya hapo chini kabla au ifikapo **tarehe 05/06/2024, Saa 9:30 Alasiri**.

Wote mnakaribishwa.

HUSNA TONI  
MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
NYANG'HWALE.